**HOTUBA YA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA HAFLA YA KUKABIDHI BOTI ZA UVUVI NA VIZIMBA VYA KUFUGIA SAMAKI**
**TAREHE 30 JANUARI 2024 - MWANZA**

- *Mheshimiwa Abdallah Ulega (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi;*
- *Mheshimiwa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi*
- *Mheshimiwa Jumaa Aweso (Mb), Waziri wa Maji;*
- *Waheshimiwa Naibu Mawaziri wote waliopo, wakiongozwa na Mheshimiwa Alexander Mnyeti (Mb), Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi;*
- *Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa CCM, Wenyeviti wa Mikoa ya Kanda ya Ziwa,*

*Wajumbe Halmashauri Kuu wote, Kamati za Siasa za Mikoa na Wilaya;*

- *Viongozi wengine wa Vyama vya Siasa;*
- *Mheshimiwa Amos Makala, Mkuu wa Mkoa wa Mwanza pamoja wa Wakuu wa Mikoa wa Mara, Geita, Simiyu na Kagera;*
- *Waheshimiwa Wabunge mliopo nasi;*
- *Prof. Riziki Shemdoe, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi;*
- *Mhandisi Luhemeja, Katibu Mkuu- OWM- Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu;*
- *Ndugu Frank Nyabundege, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo;*
- *Makatibu Tawala wa Mikoa ya Mwanza, Mara, Simiyu, Geita na Kagera;*

- *Wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mwanza;*
- *Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya za Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla wenu;*
- *Waheshimiwa Wastahiki Mameya wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza na Manispaa ya Ilemaela*
- *Bi. Agnes Meena, Naibu Katibu Mkuu Uvuvi;*
- *Prof. Daniel Mushi, Naibu Katibu Mkuu Mifugo;*
- *Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo, Taasisi na Watumishi wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi;*
- *Ndugu yetu Kutoka Zanzibar anayemwakilisha Waziri wa Uchumi wa Buluu;*
- *Wadau wa Maendeleo;*
- *Viongozi wa Dini pamoja na Machifu wenzangu na Wazee wa Mwanza;*

- *Wawakilishi kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali;*
- *Wavuvi na wafugaji wa samaki;*
- *Wadau wa Uvuvi na Ukuzaji Viumbe Maji;*
- *Wanahabari;*
- *Wanangu wa bodaboda mliopo hapa, Vikundi vya burudani;*
- *Wageni Waalikwa, wana Mwanza na wana Kanda ya Ziwa;*
- *Mabibi na Mabwana.*

*Uvuvi Oye!*

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

## ***Utangulizi***

***Ndugu Wananchi;***

Kwanza nami nianze kuongeza sauti yangu kwenye kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia afya na kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo.

Lakini pili, nimshukuru Mheshimiwa Abdallah Ulega (Mb), Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika hafla hii ya kukabidhi boti za kisasa za uvuvi na vizimba vya kufugia samaki kwa wafugaji wa Kanda ya Ziwa.

Kipekee kabisa, niwashukuru wenyeji wetu Mkoa wa Mwanza, kwa ukaribisho mzuri, kama kawaida yenu. Wanangu wa bodaboda niliwaona, mlinipokea kwa bashasha zote, nawashukuru sana! ***Mwanza Oye!***

Niwashukuru pia wananchi wote mliojitokeza kushuhudia tukio hili muhimu katika sekta ya uvuvi hapa Mwanza. Sekta hii ina mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi na uchumi wa mtu mmoja mmoja, hivyo mmefanya vizuri kujitokeza kwa wingi wenu.

## ***Mchango wa Sekta ya Uvuvi Kiuchumi***

***Ndugu zangu;***

Nchi yetu imebarikiwa kuwa na ukanda mrefu wa bahari katika Bahari ya Hindi; tunayo maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa; tumebarikiwa mito mikubwa kwa midogo, maeneo oevu na mabwawa ya asili. Aidha,  rasilimali hizi zina wingi wa bioanuawi na

viumbe maji, na huu ndio msingi wa shughuli za kiuchumi zinazohusisha uvuvi na ukuzaji viumbe maji.

Pamoja na wingi wa rasilimali maji hizi, bado Sekta ya Uvuvi nchini inatoa mchango mdogo wa **asilimia 1.8** tu kwenye Pato la Taifa. Huu ni mchango mdogo sana ukilinganisha na rasilimali za maumbile alizotupa Mungu. Kwa mujibu wa takwimu tulizonazo, Tanzania ina wavuvi takriban **197,763** na wakuzaji viumbe maji **34,057**. Aidha, mnyonyoro mzima wa thamani katika sekta ya uvuvi umeajiri karibu watu **milioni 6** hivi, ambapo ni idadi kubwa lakini tuna haja ya kuongeza ya walioajiriwa kwenye sekta hii. Kwa muda mrefu, kiwango cha ukuaji wa sekta hii kimeendelea kuwa chini ya asilimia 4 kwa mwaka.

Kati ya mwaka 2022 na 2023, tulijitutumua kidogo, mauzo ya mazao ya uvuvi nje ya nchi yaliongezeka kwa **asilimia 7**. Lakini kama nilivyosema, bado tunaweza kufanya vizuri zaidi ya hapa. Hata hivyo, ukuaji huo haulingani na fursa na thamani halisi iliyopo kwenye sekta hii. Hivyo, tukiongeza tija kwenye sekta hii, bila shaka kutakuwa na manufaa makubwa zaidi kwa nchi na wananchi waliojiajiri kwenye sekta hii. Hapa nataka niwashukuru wote waliojitokeza hapa waliojiajiri katika sekta hii, nataka pia niwapongeze wote walionufaika leo, na wale ambao bado, ahadi yangu kwenu, tutaendelea kufanya kama tuliyoyafanya ya leo.

***Mkakati wa Kukuza Sekta ya Uvuvi***

***Ndugu Wananchi;***

Nataka niunganishe tulichofanya leo na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, inayotutaka ***kuhakikisha tunatumia rasilimali zetu katika kuongeza ajira, kipato na ustawi wa jamii***. Kwa kuzingatia hilo, Serikali imedhamiria kuleta mageuzi na maboresho makubwa kwenye Sekta ya Uvuvi. Mageuzi haya yanalenga kuendeleza sekta hii na kuongeza fursa za ushiriki kwa wananchi wengi zaidi. Ili kufikia lengo hilo, Serikali imetoa kipaumbele katika kuongeza uzalishaji wenye tija, kukuza sekta na kuongeza mchango wa sekta ya uvuvi nchini.

Hatua za awali kabisa zilizochukulawa katika kuinua sekta ya uvuvi nchini, ni kuimarisha utendaji wa

Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili uendane na dhamira yetu ya mageuzi tuliyoyakusudia. Kwa muda mrefu nimekuwa nikipiga kelele na Wizara hii, lakini kila ninavyowasukuma hawaendi, sioni kile ninachokitaka. Nikaamua kufanya mageuzi, niliyemuweka nikamwambia sasa nakupa miezi sita, nione umefanya kama Kilimo walivyofanya. Nakushukuru sana Waziri, umejitahidi sana. Nakushukuru wewe, Katibu Mkuu na watendaji wenu ndani ya sekta hii, mmefanya vizuri.

Lakini niliitaka Wizara ijiwekee muundo mzuri ambao utawawezesha kufanya kazi yao na kubuni mbinu na mikakati itakayowezesha **kuongeza idadi ya wazalishaji kibiashara, na wafanyabiashara ndani na**

**nje ya nchi katika sekta hii**. Sasa leo, Waziri ameleta ombi la kuwa na Wakala wa Uvuvi, sasa Waziri ombi nimelisikia lakini ningependa sana mje mfanye Wasilisho kwenye Baraza, ili Serikali tutambue mnataka nini haswa, na kama tunakubali au tunakataa, lakini tuwe tumeelewa mnataka nini. Kwa sasa natambua kwamba, Maafisa Uvuvi wote wako chini ya TAMISEMI. Kwa hiyo Muundo mnaokuja nao mtambue na hilo pia, mnajiunganisha vipi na TAMISEMI ili kutoathiri ugatuaji wa madaraka kwenye Serikali za Mitaa. Kwa hiyo, nikutake Mheshimiwa Waziri uje ufanye Wasilisho, halafu kwa pamoja tufanye maamuzi. Lakini niseme tu, nimefurahi kwamba, Wizara inaendelea kutekeleza maelekezo yangu niliyoyatoa.

*Ndugu zangu;*

Tukiangalia matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022 yanabainisha kwamba, idadi kubwa ya wananchi wa Tanzania ni vijana na wanawake. Hao ndio kundi linaloongoza kushiriki kwenye ajira zisizo rasmi. Kwa muda mrefu Sekta hii ya Uvuvi imekuwa kwenye ajira zisizo rasmi. Hatua tunazozichukua sasa ni kurasimisha ajira hizi, zitambulike, tuwe na kanzidata ya wavuvi, wakuzaji viumbemaji na wote wanaoshughulika kwenye sekta hiyo pamoja na wachakataji wa mazao hayo ya uvuvi. Kwa hiyo tunakwenda kuirasimisha sekta hii, na tuwaondoe wavuvi na wote walioko kwenye sekta hii kwenye shughuli ya kujikimu waende kwenye shughuli

ya kibiashara. Ndio maana nikasema sekta hii, inaweza kuzalisha wafanyibiashara wakubwa katika sekta ya uvuvi. Tunafanya jitihada za makusudi za kuwawezesha vijana na wanawake kupata zana na nyenzo za kisasa ili waweze kurasimisha. Tulichokifanya leo ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wetu huo.

## ***Boti na Vizimba Kuongeza Tija***

***Ndugu zangu,***

Leo nimezindua ugawaji wa boti **160** za uvuvi wa kisasa ambazo kati yake boti **55** zitagawiwa ndani ya Kanda ya Ziwa na wanufaika ni kama Mheshimiwa Waziri alivyotueleza. Wito wangu kwa walionufaika, ni

kuzitunza boti hizi, kutunza vifaa hivi, kutumia vyema vifaa vilivyotolewa, ili kuongeza tija katika sekta hii.

Uzoefu unatuonesha mahali kwingine tunapofika hatua hizi, tunatoa vifaa na kila kitu, vifaa vya kisasa kabisa, kinachotokea kwenye makundi yenu huko ni kwenda kugombana, ni kwenda kulumbana. Tunaishia ugomvi na kesi, na vifaa hivi haviendi kuzalisha. Niwaombe sana, nendeni kakaeni vyema, jipangeni na Sekretariati za Wilaya na Mikoa visaidieni vikundi, kampuni na wote waliopata vifaa hivi waende wakafanye vyema, wakaongeze tija kwenye uzalishaji wa mazao ya uvuvi.

***Maombi***

Natambua kwamba idadi ya mahitaji ni kubwa kuliko tulichokifanya leo, kama nilivyosema, ahadi yangu ni kwamba, tunakwenda kuongeza idadi ya vifaa na tutarudi awamu nyingine kutoa vifaa kwa wale wengine ambao hawajapata. Kama alivyosema mnufaika leo, tayari dirisha la pili limeshachukua mahitaji, wanasubiri kugawiwa, tunakwenda kuona jinsi ya kufanya, ili hawa waliojiandikisha awamu ya pili na wenyewe waweze kunufaika na vifaa hivi.

Lakini pia kuna maombi ambayo msoma risala aliyasema, maombi kama uwepo wa miundombinu, lakini pia kiwanda cha kuzalisha chakula cha samaki pamoja na kuchakata barafu. Sasa, kwa kawaida miradi

hii, ikifanya vizuri huvutia sekta binafsi. Ni imani yangu kwamba, wanufaika, wafugaji na wavuvi, mkifanya vizuri katika mzunguko wa kwanza, basi wafanyabiashara watakuja wenyewe kuweka miradi uzalishaji wa chakula na barafu, karibu na maeneo yenu. Kwa hiyo kwetu sisi ni kuendelea kupigia debe ili sekta binafsi nayo ije kuwekeza yale ambayo mmeyataka.

Pamoja na hayo, niseme kwamba, mradi huu unaenda na miundombinu mingine, na imesemwa hapa na Waheshimiwa Wabunge. Kwamba, kwa upande wa Nyamagana, tunakwenda kujenga soko la kisasa, ambalo ndani yake kutakuwa na miundombinu ya kuhifadhia samaki. Kwa hiyo, hilo ni moja, lakini soko lile,

litazungukwa na barabara ya kilometa 3, ambayo itakuwa ni rahisi kufikika.

Kwa upande wa Ilemela, na wenyewe kwa sababu wavuvi wengi wako kule, tunakwenda kuziboresha barabara, kilometa 12 ili kuwe na urahisi wa kupeleka mazao kunakohitajika. Kwa hiyo kwa upande wa maombi, niseme hivyo kwa ufupi.

**Kuhusu vizimba**

Niseme kuhusu vizimba vilivyogawiwa leo kwa mzunguko mmoja, vinaweza kuzalisha kati ya **tani 3** hadi **5.1** inategemea na ukubwa wa kizimba. Wakati mvuvi wa kawaida ukimpa eneo ambali kizimba kinakaa,

anaweza kupata samaki, si zaidi ya kilo 1 tu. Kwa hiyo uvuvi wa vizimba, ni uvuvi wa kisasa na ni uvuvi ambao utaleta tija kwa haraka. Kupitia uvuvi wa vizimba, mfugaji wa samaki anaweza kupata hadi kilo 20 katika eneo la mita 1 ya mraba. Sasa kilo 20 tukifuga vizuri ni samaki mmoja na pengine kupita hapo. Wakati nakabidhi boti nilionesha samaki aina ya sangara mkubwa ana kilo 45, huyo ametoka ziwani, lakini anaweza akatoka ndani ya kizimba pia kama tutafuga kwa kuzingatia kanuni za ufugaji bora wa samaki. Tunaweza tukamtoa ndani ya kizimba. Nimeambiwa samaki yule mmoja, anaweza kuuzwa hadi Shilingi 700,000. Kwa hiyo wafugaji na wakuzaji viumbe maji kazi ni kwenu. Serikali tumeshajenga miundombinu, tumeshaweka mazingira

wezeshi, kazi kwenu kuzalisha ili Serikali nasi tuje awamu ya pili kutumia mazao mtakayoyazalisha.

Nitumie fursa hii kuipongeza Wizara kwa kubuni Programu hii itakayokuwa na manufaa makubwa kwa wavuvi na wafugaji wa samaki. Boti za kisasa tulizozigawa leo zitawawezesha wavuvi kwenda maeneo ya maji ya kina kirefu ili kupata samaki wengi zaidi, na hivyo kuongeza tija kwenye shughuli zao.

Ujumbe wangu kwa wavuvi na wafugaji wa samaki, mliopo hapa na mnaofuatilia kote nchini, ni kwamba, tunachofanya leo ni sehemu tu ya mpango huu. Shabaha yetu ni kufanya mradi huu uwafikie wavuvi wengi zaidi

kupitia vikundi vyenu, au mmoja mmoja atakayeonesha uwezo mkubwa na tutafanya hivyo kwa awamu. Tulianza kule Kilwa, tumekuja Mwanza na Kanda ya Ziwa, tutakwenda maeneo mengine ya Pwani, tutarudi tena labda Kigoma kule, kwenye Ziwa Tanganyika, tutakwenda Nyasa pia. Tutakwenda kuwaona wavuvi wote walioko katika maeneo hayo.

Kwa upande wa walionufaika na mradi huu, kama nilivyosema, wito wangu ni kuwaomba watunze vifaa hivi walivyokopeshwa. Matarajio yetu baada ya kupata zana hizi, ni kwamba mtaongeza bidii na maarifa zaidi na kuhakikisha ubora unazingatiwa. Ni lazima tulinde afya za walaji, lakini pia tusijiharibie masoko ya bidhaa hizi nje ya nchi au kimataifa.

***Ndugu zangu,***

Uendelevu wa mradi huu kwa kiasi kikubwa unategemea uaminifu wenu. Ili wenzenu katika maeneo mengine ya nchi yetu wanufaike na fursa hii kama nilivyowataja, ni lazima ninyi wanufaika wa awali mfanye marejesho kama mlivyokubaliana. Najua kabla ya kupewa, mliwekwa kitako, mkaelezwa kwamba huu ni mkopo na ni vizuri kwamba mkopo usio na riba, Serikali inatoa mkopo usio na riba, lakini mfanye kazi, mrudishe ili na wengine waweze kunufaika na mambo haya. Uaminifu wenu pia utaongeza imani ya wakopeshaji wengine.

Leo tumeanza na TADB, lakini mkirudisha vizuri, wengine wakiona TADB ifanya vizuri, makusanyo ni mazuri, wengine wataingiza fedha TADB ili ikopeshe watu wengi zaidi. Kama nilivyosema, mkopo huu sio *kausha damu*, ni mkopo ambao unafanya kazi unalipa kilekile ulichokopeshwa. Hivyo timizeni wajibu wenu wa kulipa deni, ***kwani dawa ya deni ni kulipwa.*** Tusije kuanza kufukuzana huko, mara kikundi hakipo, kampuni imefilisika, sijui nani hayupo. Twendeni tukafanye kazi, tuzalishe, tulipe mikopo tuliyochukua.

## ***Mikakati Zaidi Katika Sekta ya Uvuvi***

***Ndugu Wananchi;***

Serikali imejipanga kikamilifu kuchochea ukuaji wa Sekta ya Uvuvi kupitia Mipango na Programu mbalimbali ili kuongeza mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa.

Miongoni mwa mipango hiyo ni utekelezaji wa Mradi wa kielelezo ikiwemo ununuzi wa meli za kisasa za uvuvi katika Bahari Kuu, ujenzi wa bandari za uvuvi katika maeneo ya Kilwa Masoko Mkoani Lindi na kule Bagamoyo. Bandari hizo zitakapokamilika zitakuwa miongoni mwa bandari kubwa na za kisasa katika Ukanda wa Afrika Mashariki. Kwa hiyo tunajipanga hivyo. Kilwa tayari tumeanza na Bagamoyo tutaanza hivi karibuni.

Miradi mingine ni pamoja na ujenzi wa masoko ya samaki ya kisasa. Moja litakuwa hapa Nyamagana, tutajenga mialo ya kupokelea samaki na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya uvuvi ili kupunguza upotevu baada ya kuvunwa. Vilevile, tunakwenda kuainisha maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki kwa vizimba katika maziwa makuu, kama nilivyosema tutakwenda pia Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa, kote tutakwenda kueneza uvuvi wa aina hii. Ujenzi wa vituo vya kuendeleza ukuzaji viumbe maji na mashamba darasa ya ufugaji wa samaki, yote ni katika mipango tunayopanga kuitekeleza.

Mpango mwingine ni wa kuwawezesha vijana na wanawake kupitia fursa zinazopatikana katika sekta ya uvuvi unaojulikana kama Jenga Kesho Iliyo Bora katika

Mifugo na Uvuvi (**BBT-LIFE)**. Katika mwaka 2022/2023 vijana wapatao 200 wameshapatiwa mafunzo maalum kwa ajili ya kuanzisha biashara na makampuni yatakayotumia rasilimali za uvuvi na ukuzaji viumbe maji, na hawa ndio wanufaika tunaowaona leo, lakini pia katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tumewafundisha na kuwapa zana ili kuongeza ajira na kipato cha mtu mmoja mmoja na hatimaye Taifa kwa ujumla.

Mwaka wa fedha 2023/24 vijana wengine 300, kama alivyosema, msoma risala, wameshachaguliwa kujiunga na mafunzo hayo. Wahitimu watapatiwa kama walivyopatiwa hawa, mikopo yenye masharti nafuu na mtaji wa kuanza uwekezaji kupitia vikundi na makampuni yao. Imani ya Serikali ni kwamba mpango

huu u**taongeza kasi ya kukuza vijana wafanyabiashara wapya kwenye sekta hii ya uvuvi** na *In shaa Allah*, watapatikana. Inawezekana wewe kijana unayenisikiliza hapa uwanjani au unayenitazama au kunisikiliza kupitia vyombo vya habari ukawa mmoja wa watakaonufaika baadaye. Jambo muhimu ni kuwa na nia na dhamira ya kubadili maisha yako. Ukiweka nia hiyo na dhamira, Serikali iko pamoja na wewe, tutakuwezesha, utabadilisha maisha yako.

## ***Baadhi ya Masuala Makhsusi Kuhusu Uvuvi***

***Ndugu zangu,***

Kuendana na nilichokifanya leo, na kwa sababu niko Mwanza, nataka nitumie fursa hii kuzungumzia masuala

matatu yanayoendana na kushamiri au kukua kwa sekta ya uvuvi, ambayo naamini yanaigusa Mwanza lakini yanaweza kugusa Kanda ya Ziwa nzima.

Mambo yenyewe ni kwanza, **kutumia uwanja wa ndege wa Mwanza kusafirisha mazao ya Uvuvi.** Najua haipendezi uwanja uko hapa, mazao yanayovunwa Tanzania yakasafirishwa kupitia uwanja wa ndege wa nchi nyingine. Haipendezi hata kidogo! Kwa hiyo nilitoa maelekezo kwa Mkuu wa Mkoa, pamoja na mambo mengine, nilimtaka afuatilie, kufanya maboresho ya Uwanja wa Ndege kwa kuweka jengo jipya la abiria na Waziri yuko hapa wa Uchukuzi miundombinu ya kuhifadhi samaki (*coldroom*).

Uwanja huu ulisuasua kule nyuma. Lakini nafurahi kwamba, nilipoingia Mwanza, Mkuu wa Mkoa ameniambia, masuala ya ujenzi wa *coldroom*, tayari yameanza kuchukuliwa hatua, na ujenzi utaendelea vizuri hivi karibuni. Lakini kwa upande wa ujenzi wa jengo la abiria na uendelezaji wa kiwanja cha ndege cha Mwanza, Waziri amenisikia na najua yuko katika hatua kadhaa za kumalishaa jengo la abiria na kufanya mambo mengine.

**Jambo la pili** ni **upatikanaji wa umeme** wa uhakika kwa viwanda vya kusindika mazao ya uvuvi, na viwanda vingine. Kama nilivyosema kwenye Hotuba yangu ya kufunga mwaka kwamba, tatizo la upungufu wa umeme tunaendelea kulipatia ufumbuzi. Kwa hiyo,

baada ya muda si mrefu tutakuwa tumepunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la kukatika katika kwa umeme.

**Jambo jingine ninalotaka kulizungumzia ni kuhusu Soko la Mazao ya Uvuvi.** Nataka hapa niseme kwamba, kwa wale wanaofanya kazi ya uvuzi, ukuzaji wa viumbemaji, na wachakataji wa mazao ya uvuvi, fanyeni kazi kwa nguvu sana. Soko la mazao haya ni kubwa duniani. Inatarajiwa kwamba, idadi ya watu duniani itaongezeka kufikia watu bilioni 9 ifikapo mwaka 2030. Lakini idadi hiyo itakwenda kuongezeka zaidi, kufikia watu bilioni 10 ifikapo mwaka 2050. Kwa maana hiyo, inatarajiwa vilevile, kiwango cha utumuaji wa mazao ya baharini, yamekua kutoka wastani kilogramu 10 kwa mtu kwa mwaka miaka ya 1960, hadi kilo 20 kwa mtu kwa

mwaka kufikia miaka ya 2010. Inakisiwa kuwa, kiwango hicho kitaendelea kukua. Matumizi ya mazao ya baharini yataendelea kukua, kama alivyosema hapa Waziri, kwamba, ni sehemu moja ya lishe inayotegemewa duniani. Kwa maana hii, soko la mazao ya uvuvi lipo la kutosha duniani kote.

Kwetu sisi Tanzania, kama Taifa, tujipange ili tuweze kutumia vizuri fursa ya soko hilo kwa kufanya uzalishaji zaidi unaofuata kanuni bora za uzalishaji na uchakataji wa mazao hayo, ili tuwe tuna soko kubwa duniani, na Tanzania iingie miongoni mwa nchi zinazoweza kuuza mazao ya baharini kwa kiasi kikubwa. Niwaombe sana Ndugu Zangu, fuateni Kanuni zote za

uzalishaji, usafi na mambo mengine ili tuweze kusafirisha kwa wingi zaidi.

***<u>Maelekezo mahususi</u>***

***Ndugu Zangu;***

Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta ya uvuvi katika Uchumi wa taifa letu, rasilimali za uvuvi zinapaswa kusimamiwa, kuendelezwa na kutumiwa kwa njia endelevu. Hivyo, nitumie jukwaa hili kuelekeza yafuatayo:-

***Mosi,*** Wizara ya Mifugo na Uvuvi ifuatilie kwa karibu zaidi, maendeleo ya walionufaika na vifaa tulivyogawa leo na kutoa ushauri wa kitaalam. Nilikuwa naongea na Waziri akaniambia, mizao mitatu ya awali,

Wizara itakuwa bega kwa bega na wazalishaji na wachakataji. Kwa hiyo niombe msipunguze lolote katika mpango huo. Mizunguko mitatu ya awali kwa kutumia vizimba lakini boti pia, muwe karibu sana na wanufaika ili muweze kuwaongoza. Aidha, Wizara iendelee kutenga bajeti kwa ajili ya wanufaika wengine kipaumbele kikiwa vikundi vya wavuvi na wakuzaji viumbe maji wadogo na wa kati. Lakini kwa sababu tunashughulika na benki, Wizara, mnaweza mkatafuta mtaji, mkauweka benki, na mkaitaka benki kukopesha, mtaji mliotoa ikawa ndio dhamana kwa wanaokopeshwa. Hilo litakwenda kufanya mikopo iende haraka.

***Pili,*** shughuli zote za uvuvi nchini lazima ziendeshwe kwa kuzingatia sheria, taratibu na Kanuni tulizojiwekea ili

rasilimali za uvuvi ziwe endelevu kwa kizazi cha sasa na kizazi kijacho. Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) shirikianeni na Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri husika kudhibiti na kutokomeza vitendo vya uvuvi haramu kwa kuwachukulia hatua kali za kisheria wanaokiuka taratibu za uvuvi salama.

Lakini ninaposema kuchukua hatua kali, nataka niseme jambo moja**, uchomaji wa nyavu** na zana za uvuvi unaolenga kukabiliana na uvuvi usiotakiwa unarudisha nyuma maendeleo ya uvuvi. Lakini pia inajenga chuki kati ya wavuvi na Serikali kwa kuchukua nyavu zao na kuzichoma. Tunachokifanya sasa, utoaji wa vifaa vya kisasa, nina hakika nyavu zilizotolewa leo sio nyavu za makokoro, ambazo zinakatazwa, ni nyavu nzuri. Kwa

hiyo, naomba Wizara, muongeze kasi katika kusambaza nyavu zile, kwa njia ya mikopo, ili wavuvi wasitumie nyavu zinazokatazwa. La pili ni elimu kwa wavuvi wetu, muwe karibu sana na wavuvi, kama mtaunda huo Wakala wa Uvuvi, kama mtatushawishi kwenye Baraza, basi Wakala uwe karibu sana na wavuvi, kutoa elimu ya kutosha kwamba, uvuvi wanaofanya wa makokoro, unamaliza rasilimali zetu. Mkitumia makokoro, mnakwenda kumaliza rasilimali ile, na vifaa vya kisasa tunavyotoa havitaleta tija iliyokusudiwa. Kwa hiyo, niombe sana, elimu kwa wavuvi iendelee, badala ya kukusanya nyavu na kuzichoma, lakini lazima wachukuliwe hatua za aina flani, ili kukomesha uvuvi haramu.

Kwa upande wa wavuvi wachache wanaofanya vitendo hivyo, niwatake mtimize wajibu wenu kwa kuacha vitendo hivyo vinavyomaliza mazalia ya rasilimali hizo. Kamati za wavuvi katika maeneo mbali mbali lindeni maeneo yenu ili kazi hii muweze kuirithisha kwa vizai vijavyo ikiwa katika mfumo endelevu. Wazee wetu wangemaliza, sisi leo tusingegawa vifaa hivi, kwenda kuvuna rasilimali zilizopo. Kwa hiyo lindeni maeneo yenu. Hasa nyinyi wa vifaa vya kisasa, lindeni wanaowaharibia uzalishaji wa rasilimali hizi.

***Mwisho***, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kupitia Kituo cha Uwekezaji ihakikishe inatangaza fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Sekta ya Uvuvi na Uchumi wa

Bluu ili tuongeze thamani mazao ya uvuvi na viumbe maji ili tuweze kutengeneza ajira zaidi kwa vijana wetu.

## ***Hitimisho***

Nikihitimisha Hotuba yangu, niruhusuni kwa mara nyingine tena, nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wadau wetu wa maendeleo kwa namna wanavyoendelea kushirikiana na Serikali katika kubuni, kuandaa na kutekeleza mikakati, programu na mipango mbalimbali inayohusu sekta ya uvuvi. Tunaendelea kuwakaribisha kwa mashirikiano zaidi kwenye sekta hii muhimu.

Programu tuliyoizindua leo imekuja wakati muafaka ambapo Serikali inaendelea kuleta mapinduzi makubwa

katika sekta zote ikiwemo sekta ya uvuvi. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kazi kubwa anayofanya, lakini nimtake asilewe sifa na kubweteka. Nimewasifu sana leo hapa, msiende kubweteka. Kazi kubwa bado inatakiwa kufanyika kwenye sekta ya mifugo na uvuvi. Ninaposema nataka tupate wafanyabiashara mahiri kwenye sekta hizi, ninamaanisha. Ninaomba hilo, muishi nalo na iwe ndio kauli mbinu yenu, kwamba tunakwenda kuzalisha wafanyabiashara mahiri kwenye sekta ya uvuvi na mifugo pia. Kama mtakwamwa, Waziri unajua kwamba milango yangu iko wazi, njoo tushauriane, na mtendaji wako tuone tunalipeleka vipi jahazi hili.

Baada ya kusema hayo, niwashukuru sana kwa kunisikiliza.

Niseme Mungu aibariki, Afrika yetu, Mungu aibariki Tanzania; Mungu awabariki Watanzania wote, na

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.